BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUANZISHA MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA, KAZI, MAJUKUMU NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambae ametujaalia neema ya uhai na uzima na kutuwezesha kukusanyika hapa kutekeleza wajibu wakuwatumikia wananchi pamoja nakuliongoza vyema gurudumu la maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, yenye utulivu, na yenye umoja na mshikamano mkubwa, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wake ambao asilimia kubwa ni wakwezi na wakulima kuweza kutekeleza majukumu yao kwa amani na mshikamano. naiombea Nchi yetu kudumu katika hali ya amani na utulivu kwani bila ya amani hakuna maendeleo yatakayopatikana.

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe pamoja na wasaidizi wako, Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza kwa namna mnavyoliendesha Baraza kwa umahiri mkubwa, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie hekma na busara katika jukumu lenu la uongozi ili tuweze kutekeleza vyema wajibu wa chombo hiki.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile napenda kumpongeza na kumshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji wake mzuri wa majukumu yake ambayo

yamepangwa vizuri kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 2025. Pia, kujali kwake Utawala wa Sheria na Utawala Bora ambao umepelekea maamuzi ya kuifuta Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya, Nam. 9 ya mwaka 2009 na kutunga Sheria mpya itayojulikana kama Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ambayo inaendana na kasi ya sasa ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya na yenye uwezo kamili wa kukabiliana na uhalifu huu.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, shukurani za pekee ziwaendee Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na Mkurugenzi wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, Zanzibar kwa mashirikiano yao makubwa katika kuhakikisha Mswada huu umekamilika na umekua na tija kwa Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika;** kwa dhati kabisa, Kamati inawashukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na wadau wote waliochangia mswada huu kwa namna tofauti. Imani yangu kuwa michango yao mizuri waliyotoa itasaidia sana katika kuufanya Mswada huu kuwa bora zaidi. Vilevile, napenda kuwahakikishia kwamba maoni na ushauri wao umezingatiwa na Kamati wakati ilipokaa na Wizara ili kupatiwa ufafanuzi kuhusu Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika;** naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo Kamati yetu imeyafanya na pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ilikutana na Wizara ya Nchi OR - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora siku ya **Jumanne**, tarehe **30 Novemba, 2021** na kuupitia Mswada huu kifungu

kwa kifungu pamoja na kufanya marekebisho ya kimantiki na kisarufi. Vile vile, Wizara iliwasilisha katika kikao hicho Mapendekezo ya Marekebisho ya Mswada huu katika vifungu vya 13,15 na 24.

**Mheshimiwa Spika,** naomba niende moja kwa moja katika baadhi ya vifungu ambavyo Kamati imevifanyia marekebisho, kama ifuatavyo:-

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeelezwa kwamba mapambano ya Matumizi ya Dawa za Kulevya Zanzibar yamedumu kwa miongo kadhaa ambapo mafanikio mbali mbali yameweza kupatikana licha ya jamii kuathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na janga hili. Hata hivyo, mnamo mwaka 2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza lako Tukufu lilitunga sheria mpya No. 9 ya 2009 iliyojulikana kama Sheria ya Kudhibiti Dawa za Kulevya lakini Sheria hii imeonekana kuwa na mapungufu ndani yake kwani Sheria hiyo haitowi uwezo kamili wa kudhibiti na kupambana na matumizi ya dawa za kulevya, usafirishaji, ugeuzaji wa kemikali bashirifu na udhibiti wa dawa tiba.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Mamlaka itakayoanzishwa itakuwa ni chombo kinachojitegemea chenye uwezo wa kushitaki na kushitakiwa na kitakuwa kimejumuisha mambo yote yanayohusiana na chombo chenye kujitegemea, Kamati inshauri kifungu cha 13(1) kurekebishwa kwa kuingizwa maneno "Uratibu wa" baina ya neno "ya" na neno "kudhibiti". Hivyo aya hii itasomeka kama ifuatavyo:

"kutakuwa na Kamati ya Uratibu wa Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mkoa katika kila Mkoa".

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, Kamati inapendekeza na kushauri kufutwa kwa aya (e) ya kifungu cha 13(2) eneo ambalo limetoa fursa kwa Mkuu wa Mkoa kuteua watu wawili watakaoingia katika Kamati ya Mkoa. Kamati imeshauri kufanyika mabadiliko hayo ili kutoa fursa kwa Mamlaka kutekeleza majukumu yake pasi na kuingiliwa na Mamlaka nyengine kama

vile Mamlaka za Mikoa na Wilaya. Aidha, Kamati inashauri kifungu kidogo cha 13(3) kufutwa na badala yake kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"Katibu Tawala wa Mkoa atakuwa Katibu wa Kamati".

**Mheshimiwa Spika,** Katika Sehemu ya Tatu ya Mswada huu ambayo imeweka Muundo wa Baraza la Taifa la Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya limetaja wajumbe mbali mbali ambao watashiriki kwa nafasi zao kutokana na umuhimu wa nafasi hizo katika kupambana na madawa ya kulevya, wote wakiwa na dhamira ya kukamilisha malengo yaliyokusudiwa. Hivyo basi, Kamati inashauri katika Kifungu cha 15 (1) kurekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya (l) badala ya aya (k) kama ifuatavyo:

"Waziri anayeshughulikia mambo ya Mawasiliano".

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeshauri kuingizwa kwa Waziri anaeshughulikia mambo ya Mawasiliano kutokana nayeye ndiye mwenye dhamana ya Bandari na Viwanja vya ndege ambazo ndizo sehemu kuu zinazotumika kuingizia na kutolea mizigo. Hasa tikifahamu kwamba Zanzibar ina bandari rasmi na zisizo rasmi ambapo inasadikika kuwa bandari zisizo rasmi zinatumika kupitisha madawa ya kulevya kwa kiasi kikubwa katika nchi yetu. Aidha, naomba ifahamike kuwa wakati Kamati inapendekeza suala hili kulitokea mvutano kidogo na kushindwa kufikia muwafaka juu ya marekebisho hayo.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kifungu cha 15 (9) Kamati imeshauri kufutwa na kuandikwa upya aya hiyo na kusomeka kama ifuatavyo:
"Baraza litateuwa mtu kwa ajili ya kuongoza kikao"

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inapendekeza katika kifungu cha 16(2)(c) Mfuko wa Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kupewa asilimia 100 ya mauzo ya mali yoyote iliyofilisiwa chini ya Sheria hii, ili mfuko huu upate kufanya kazi zake bila changamoto zozote za kifedha na kiutendaji,

tunaamini kupewa asilimia mia moja kutatoa ufanisi katika mapambano dhidi ya uhalifu huu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria hii ambayo inaanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kazi, Majukumu na mambo mengine ndani yake inaakisi maendeleo ambayo yamepatikana katika Mataifa mbali mbali Duniani. Kwa mfano, majirani zetu wa nchi ya Kenya ambapo kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Umoja wa Mataifa, mwaka 1998 Kenya ilikuwa miongoni mwa nchi zilizofanikiwa sana katika ukanda huu wa Kusini na Mashariki mwa Afrika katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** Sera na Sheria zenye muundo kama huu, ndiyo iliyowasaidia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo yao. Lakini pia, nchi zilizoendela kama vile USA, Portugal, Germany na Netherlands ni miongoni mwa nchi zinazotumia Sera na Sheria yenye muundo kama huu na wamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupambana na dawa za kulevya katika nchi zao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia hotuba yangu, naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Makatibu wangu kwa mashirikiano makubwa ambayo wanatupatia katika kuendesha shughuli zote za Kamati yetu.

**Mheshimiwa Spika;** sasa naomba uwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Machano Ohman Said | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 9. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama. |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote ambao naiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati yangu inawaomba wajumbe wa Baraza hili Tukufu kwamba Mswada huu uliombele yetu waujadili na wauchangie ipasavyo na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itapunguza changamoto zinazowakabili vijana wetu ambao ndio nguzo pekee ya kulijenga Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba Kuwasilisha.

……………………..

**(Mhe. Hassan Khamis Hafidh)**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**